

02.04.2026

TANGAZO LA ZABUNI YA MATENGENEZO YA MAGARI YA KCU (1990) LTD
MSIMU 2026/2027

Zabuni na: **KCU/NC/2026/2027/02**

1. KCU (1990) LTD inayo magari yake yanayotumika kwa shughuli mbalimbali za kiofisi, na kwa kuwa magari hayo yanahitaji matengenezo ya mara kwa mara hivyo imetenga fedha kwa ajili ya kuingia makubaliano ya kimkataba na mtoa huduma ya matengenezo ya magari makubwa na madogo kwa msimu 2026/2027.
2. Kampuni/Shirika/Mtu binafsi anayetambulika anakaribishwa kuleta maombi ya zabuni hii ili kutoa huduma ya kutengeneza magari makubwa na madogo ya KCU.
3. Mwombaji aambatishe nakala ya leseni ya utengenezaji wa magari makubwa na madogo.
4. Mwombaji awe na Gereji/eneo maalumu la kudumu la kutengeneza magari
5. Mwombaji aambatishe nakala zinaonesha vielelezo vya kazi alizowahi kufanya na uwezo wake wa kupata vipuri vya magari, makubwa na madogo.
6. Ombi la zabuni liwe na jina, anwani halisi ya mwombaji na mahali Ofisi ilipo.
(Physical address)
7. Maombi yaambatane na ada ya TShs. 200,000/= ambazo hazitarejeshwa kwa mwombaji. Fedha hizo zilipwe kupitia A/C Namba **01J1055955002 General A/C**
8. Tathmini itafanywa kwa kuzingatia vigezo 3-7 vilivyo tajwa hapo juu.
9. Bahasha ya maombi ifungwe vizuri kwa lakiri na kuandikwa juu yake:- **"MAOMBI ZABUNI YA MATENGENEZO YA MAGARI YA KCU MSIMU 2026/2027** _kwa anwani tajwa hapa chini,

MENEJA MKUU,
KCU (1990) LTD,
P.O BOX 5,
BUKOBA.

10. Bahasha hiyo iletwe kwa mkono katika Ofisi ya Manunuzi KCU kabla au mnamo tarehe 20.04.2026 saa 4.00 asubuhi siku ya Jumatatu na ufunguzi wa maombi yote utafanyika muda huo, waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa katika sherehe ya ufunguzi mara tu baada ya saa ya mwisho yakupokea zabuni.
11. Maombi yatakayo chelewa, maombi yasiyokamilika, maombi yaliyowasilishwa kwa njia ya kieletroniki na maombi yasiyokuwepo siku ya ufunguzi hayatahusishwa na uchambuzi wa kumpata mzabuni.
Imetolewa na;

MENEJA MKUU

